

MTU mmoja Raia wa India ameshikiliwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), kwa tuhuma za kuingia nchini na dawa kinyume na utaratibu wa sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa ZAECA, Kaimu Mkuu wa kitengo cha sheria, mikataba, mashirika ya umma na urejeshajimali, alisema mtu huyo anaesadikiwa kuwa ni mfanyabiashara anajulikana kwa jina la **Rahimu Hudda (37)**.

Alisema mtu huyo alikamatwa katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, akitokea nchini Mumbai India, akiwa na mabegi manne ya dawa. “Kwa mujibu wa kifungu cha 45 cha sheria namba moja ya 2012 sheria ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar inatoa kosa kwa mtu yeyote anaeingiza bidhaa nchini pasi na kufuata taratibu na sheria zilizowekwa atakuwa amefanya kosa,”

Hata hivyo, alisema uchunguzi wa kitaalamu juu ya dawa hizo unaendelea ili kuweza kubaini kama dawa hizo ni kwa ajili ya matumizi ya binadamu na zipo salama kwa matumizi hayo. Alifahamisha kwamba jalada la mtuhumiwa huyo lipo katika hatua za uchunguzi na utapokamilika basi jalada hilo litafikishwa kwa mkurugenzi wa mashitaka (DPP), kwa hatua zaidi za kisheria.

Aidha alitumia fursa hiyo kuitaka jamii kuendelea kutoa taarifa mbalimbali pale watapobaini viashiria au minya yoyote inayohusiana na rushwa na uhujumu wa uchumi.

Sambamba na hayo, alisema vita ya rushwa haiwezi kufanikiwa bila ya kuwa na mashirikiano baina ya wananchi, watendaji wa serikali, wadau na ZAECA.